JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA MATOKEO YA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE NA KIDATO CHA PILI ILIYOFANYIKA OKTOBA/NOVEMBA 2023

**IMETOLEWA NA:**

**KATIBU MTENDAJI**
**TAREHE : 07 JANUARI 2023**

**TAARIFA YA MATOKEO YA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE NA KIDATO CHA PILI ILIYOFANYIKA OKTOBA/NOVEMBA 2023**

## 1.0 UTANGULIZI

Katika Mkutano wake wa **157** uliofanyika tarehe **07 Januari, 2023** katika ofisi za Baraza la Mitihani la Tanzania zilizopo Dar es Salaam, Baraza la Mitihani la Tanzania liliidhinisha kutangazwa rasmi kwa matokeo ya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne na Kidato cha Pili iliyofanyika mwezi Oktoba/Novemba, 2023.

## 2.0 USAJILI NA MAHUDHURIO

### 2.1 Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne

Jumla ya wanafunzi **1,693,444** walisajiliwa kufanya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne wakiwemo Wasichana **864,482** sawa na asilimia **51.05** na Wavulana **828,962** sawa na asilimia **48.95**. Kati ya wanafunzi waliosajiliwa, wanafunzi **1,545,607** walifanya Upimaji, wakiwemo Wasichana **803,647** (**92.96%**) na Wavulana **741,960** (**89.50%**). Wanafunzi **147,837** (**8.73%**) hawakufanya Upimaji, kati yao Wasichana ni **60,835** (**7.04%**) na Wavulana ni **87,002** (**10.50%**).

### 2.2 Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili

Jumla ya wanafunzi **759,799** walisajiliwa kufanya Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili wakiwemo Wasichana **405,878** sawa na asilimia **53.42** na Wavulana **353,921** sawa na asilimia **46.58**. Kati ya wanafunzi waliosajiliwa, wanafunzi **695,639** walifanya Upimaji, wakiwemo Wasichana **376,927** (**92.87%**) na Wavulana **318,712** (**90.05%**). Wanafunzi **64,160** (**8.44%**) hawakufanya Upimaji, kati yao Wasichana ni **28,951** (**7.13%**) na Wavulana ni **35,209** (**9.95%**).

## 3.0 MATOKEO YA UPIMAJI

### 3.1 Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne

#### 3.1.1 Ufaulu wa Ujumla

Jumla ya wanafunzi **1,287,934** kati ya **1,545,330** wenye matokeo sawa na asilimia **83.34** wamefaulu kwa kupata Madaraja ya **A**, **B**, **C** na **D**. Mwaka 2022 Wanafunzi waliofaulu walikuwa **1,320,700** sawa na asilimia **82.95**. Hivyo, kumekuwa na **ongezeko** la ufaulu kwa

asilimia **0.39** kwa wanafunzi waliopata fursa ya kuendelea na Darasa la Tano ikilinganishwa na mwaka 2022.

Kati ya wanafunzi waliofaulu kuendelea na Darasa la Tano, Wasichana ni **681,259** sawa na asilimia **84.79** na Wavulana ni **606,675** sawa na asilimia **81.78**. Takwimu zinaonesha kuwa, Wasichana wamefaulu vizuri ikilinganishwa na Wavulana.

Mchanganuo wa ufaulu katika madaraja mbalimbali umeainishwa katika Jedwali Na. **1**.

**Jedwali Na. 1: Ufaulu wa Jumla Kimadaraja**

| Daraja | Mwaka | Wavulana | | Wasichana | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Idadi | % | Idadi | % | Idadi | % |
| A | 2022 | 31,551 | 4.08 | 29,779 | 3.63 | 61,330 | 3.85 |
| | 2023 | 21,869 | 2.95 | 20,219 | 2.52 | 42,088 | 2.72 |
| B | 2022 | 109,557 | 14.18 | 113,506 | 13.85 | 223,063 | 14.01 |
| | 2023 | 102,860 | 13.87 | 102,134 | 12.71 | 204,994 | 13.27 |
| C | 2022 | 249,876 | 32.34 | 284,634 | 34.73 | 534,510 | 33.57 |
| | 2023 | 264,969 | 35.72 | 297,328 | 37.00 | 562,297 | 36.39 |
| A-C | 2022 | 390,984 | 50.60 | 427,919 | 52.22 | 818,903 | 51.43 |
| | **2023** | **389,698** | **52.53** | **419,681** | **52.23** | **809,379** | **52.38** |
| D | 2022 | 235,169 | 30.43 | 266,628 | 32.54 | 501,797 | 31.52 |
| | 2023 | 216,977 | 29.25 | 261,578 | 32.55 | 478,555 | 30.97 |
| A-D | 2022 | 626,153 | 81.03 | 694,547 | 84.76 | 1,320,700 | 82.95 |
| | **2023** | **606,675** | **81.78** | **681,259** | **84.79** | **1,287,934** | **83.34** |
| E | 2022 | 146,606 | 18.97 | 124,929 | 15.24 | 271,535 | 17.05 |
| | 2023 | 135,142 | 18.22 | 122,254 | 15.21 | 257,396 | 16.66 |

### 3.1.2 Ufaulu wa Shule katika Makundi ya Umahiri

Idadi ya shule katika makundi ya Umahiri inaonesha kuwa, kati ya shule zote **19,264** zenye matokeo ya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne 2023, shule **18,939** sawa na asilimia **98.31** zimepata wastani wa Daraja la **A-D** ikilinganishwa na shule **18,319** sawa na asilimia **98.27** zilizopata wastani wa madaraja hayo mwaka 2022. Hivyo, kumekuwa na **ongezeko** la asilimia **0.04** ya shule zilizopata wastani wa Daraja la **A-D** ikilinganishwa na mwaka 2022.

Mchanganuo wa idadi ya shule katika Makundi ya Umahiri umebainishwa katika Jedwali Na. **2**.

**Jedwali Na. 2: Idadi ya Shule katika Makundi ya Umahiri kwa Mwaka 2023 ikilinganishwa na Mwaka 2022**

| Daraja | 2022 | | 2023 | |
|---|---|---|---|---|
| | Idadi | % | Idadi | % |
| A [241-300] | 891 | 4.78 | 585 | 3.04 |
| B [181-240] | 1,663 | 8.92 | 1,692 | 8.78 |
| C [121-180] | 7,703 | 41.32 | 8,020 | 41.63 |
| D [61-120] | 8,062 | 43.25 | 8,642 | 44.86 |
| E [0-60] | 322 | 1.73 | 325 | 1.69 |
| **Jumla** | **18,641** | **100** | **19,264** | **100** |

## 3.2 Ufaulu wa Wanafunzi Kimasomo

### (a) Masomo ya Lugha

Ufaulu wa somo la **Kiswahili** ni asilimia **84.15** na ufaulu wa somo la **English Language** ni asilimia **72.54** ambapo katika somo la **Kiswahili** umepanda kwa asilimia **0.96** na somo la **English Language** umepanda kwa asilimia **0.82** ikilinganishwa na mwaka 2022. Aidha, katika masomo ya Lugha, Wasichana wana ufaulu mkubwa zaidi kuliko Wavulana ambapo katika somo la **Kiswahili** Wasichana wamefaulu zaidi kuliko Wavulana kwa asilimia **3.67** na katika somo la **English Language** Wasichana wamefaulu zaidi kuliko Wavulana kwa asilimia **5.20**.

### (b) Masomo ya Sayansi Jamii

Ufaulu wa somo la **Maarifa ya Jamii** na **Uraia na Maadili** ni mzuri ambapo ufaulu wa somo la **Maarifa ya Jamii** ni asilimia **86.75** na katika somo la **Uraia na Maadili** ni asilimia **85.52**. Katika masomo ya Sayansi Jamii, Wasichana wana ufaulu mkubwa zaidi kuliko Wavulana ambapo katika somo la **Maarifa ya Jamii** Wasichana wamewazidi Wavulana kwa asilimia **1.95** na katika somo la **Uraia na Maadili** Wasichana wamewazidi Wavulana kwa asilimia **1.86**.

(c) **Masomo ya Sayansi na Hisabati**

Ufaulu wa somo la **Sayansi na Teknolojia** ni asilimia **86.86** na somo la **Hisabati** ni asilimia **54.00** ambapo katika somo la **Sayansi na Teknolojia** umepanda kwa asilimia **3.67** na somo la **Hisabati** umepanda kwa asilimia **4.30** ikilinganishwa na mwaka 2022. Aidha, katika somo la **Sayansi na Teknolojia** Wasichana wamefaulu zaidi kuliko Wavulana kwa asilimia **1.63** na katika somo la **Hisabati** Wavulana wana ufaulu mkubwa kuliko Wasichana ambapo Wavulana wana ufaulu wa asilimia **55.40** na Wasichana wana ufaulu wa asilimia **52.70**.

Mchanganuo wa ufaulu wa wanafunzi katika masomo mbalimbali umeoneshwa kwenye Jedwali Na. **3**.

**Jedwali Na. 3: Asilimia ya Ufaulu kwa Wanafunzi katika Masomo Mbalimbali**

| Somo | Mwaka | Idadi | %Waliopata A [41-50] | %Waliopata A hadi B [31-50] | %Waliopata A hadi C [21-50] | % Waliopata A hadi D [11-50] | | | %Waliopata E [0-10] |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | Was. | Wav. | Jumla | |
| Kiswahili | 2022 | 1,591,755 | 11.23 | 31.96 | 62.66 | 85.60 | 80.63 | 83.19 | 16.81 |
| | 2023 | 1,544,579 | 20.83 | 43.44 | 66.63 | 85.91 | 82.24 | 84.15 | 15.85 |
| English Language | 2022 | 1,591,090 | 4.42 | 7.91 | 20.44 | 73.63 | 69.69 | 71.72 | 28.28 |
| | 2023 | 1,544,931 | 4.40 | 7.75 | 23.94 | 75.04 | 69.84 | 72.54 | 27.46 |
| Maarifa ya Jamii | 2022 | 1,591,676 | 7.43 | 27.38 | 57.41 | 85.99 | 84.11 | 85.08 | 14.92 |
| | 2023 | 1,544,782 | 2.98 | 18.01 | 54.98 | 87.69 | 85.74 | 86.75 | 13.25 |
| Hisabati | 2022 | 1,591,345 | 2.45 | 6.88 | 17.89 | 48.80 | 50.65 | 49.70 | 50.29 |
| | 2023 | 1,544,799 | 2.14 | 7.42 | 23.28 | 52.70 | 55.40 | 54.00 | 46.00 |
| Sayansi na Teknolojia | 2022 | 1,591,329 | 6.75 | 29.22 | 57.70 | 84.59 | 81.70 | 83.19 | 16.81 |
| | 2023 | 1,544,860 | 2.58 | 18.22 | 54.62 | 87.64 | 86.01 | 86.86 | 13.14 |
| Uraia na Maadili | 2022 | 1,591,632 | 13.08 | 37.00 | 61.37 | 86.13 | 83.48 | 84.85 | 15.15 |
| | 2023 | 1,544,875 | 5.70 | 33.85 | 62.33 | 86.41 | 84.55 | 85.52 | 14.48 |

## 3.3 Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili

### 3.3.1 Ufaulu wa Ujumla

Jumla ya wanafunzi **592,741** kati ya **694,769** wenye matokeo ambao ni sawa na asilimia **85.31** wamefaulu ambapo wamepata Madaraja

ya **I**, **II**, **III** na **IV**. Mwaka 2022 Wanafunzi waliofaulu walikuwa **539,645** sawa na asilimia **85.18**.
Hivyo, kumekuwa na **ongezeko** la ufaulu kwa asilimia **0.13** pamoja na **ongezeko** la idadi ya wanafunzi **53,096** sawa na asilimia **9.84** ya wanafunzi waliopata fursa ya kuendelea na Kidato cha Tatu ikilinganishwa na mwaka 2022.

Kati ya wanafunzi waliofaulu kuendelea na Kidato cha Tatu, Wasichana ni **314,949** sawa na asilimia **83.66** na Wavulana ni **277,792** sawa na asilimia **87.28**. Takwimu zinaonesha kuwa, Wavulana wamefaulu vizuri ikilinganishwa na Wasichana. Mchanganuo wa ufaulu katika madaraja mbalimbali umeainishwa katika Jedwali Na. **4**.

**Jedwali Na. 4: Ufaulu wa Jumla Kimadaraja**

| Daraja | Mwaka | Wavulana | | Wasichana | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Idadi | % | Idadi | % | Idadi | % |
| I | 2022 | 27,952 | 9.57 | 19,933 | 5.84 | 47,885 | 7.56 |
| | 2023 | 33,359 | 10.48 | 24,821 | 6.59 | 58,180 | 8.37 |
| II | 2022 | 25,643 | 8.78 | 19,643 | 5.75 | 45,286 | 7.15 |
| | 2023 | 29,359 | 9.22 | 22,635 | 6.01 | 51,994 | 7.48 |
| III | 2022 | 40,620 | 13.91 | 33,739 | 9.88 | 74,359 | 11.74 |
| | 2023 | 44,140 | 13.87 | 38,319 | 10.18 | 82,459 | 11.87 |
| I-III | 2022 | 94,215 | 32.25 | 73,315 | 21.47 | 167,530 | 26.44 |
| | 2023 | **106,858** | **33.57** | **85,775** | **22.78** | **192,633** | **27.73** |
| IV | 2022 | 161,889 | 55.42 | 210,226 | 61.57 | 372,115 | 58.74 |
| | 2023 | 170,934 | 53.70 | 229,174 | 60.87 | 400,108 | 57.59 |
| I-IV | 2022 | 256,104 | 87.67 | 283,541 | 83.05 | 539,645 | 85.18 |
| | 2023 | **277,792** | **87.28** | **314,949** | **83.66** | **592,741** | **85.31** |
| 0 | 2022 | 36,011 | 12.33 | 57,881 | 16.95 | 93,892 | 14.82 |
| | 2023 | 40,498 | 12.72 | 61,530 | 16.34 | 102,028 | 14.69 |

(a) **Ufaulu wa Shule katika Makundi ya Umahiri**

Idadi ya shule katika makundi ya Umahiri inaonesha kuwa, kati ya shule zote **5,515** zenye matokeo ya Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili 2023, shule **5,485** (**99.45%**) zimepata wastani wa Daraja la **A-D** ikilinganishwa na shule **5,187** (**98.83**%) zilizopata wastani wa madaraja hayo mwaka 2022. Hivyo, kumekuwa na **ongezeko** la asilimia **0.62** la shule zilizopata wastani wa Daraja la **A-D**

ikilinganishwa na mwaka 2022. Mchanganuo zaidi umebainishwa katika Jedwali Na. **5**.

**Jedwali Na. 5: Idadi ya Shule katika Makundi ya Umahiri kwa Mwaka 2023 ikilinganishwa na Mwaka 2022**

| Daraja | 2022 | | 2023 | |
|---|---|---|---|---|
| | Idadi | % | Idadi | % |
| A | 69 | 1.31 | 96 | 1.74 |
| B | 411 | 7.83 | 471 | 8.54 |
| C | 690 | 13.15 | 765 | 13.87 |
| D | 4017 | 76.54 | 4153 | 75.30 |
| F | 61 | 1.16 | 30 | 0.54 |

(b) **Ufaulu wa Wanafunzi Kimasomo**

(a) **Masomo ya Sayansi Jamii**

Ufaulu wa somo la **History** na **Geography** ni wa wastani ambapo katika somo la **History** ni asilimia **50.71** na katika somo la **Geography** ni asilimia **53.78**. Katika somo la **Civics** ufaulu umeimarika kutoka asilimia **31.12** kwa mwaka 2022 hadi **48.27** kwa mwaka 2023. Mchanganuo wa ufaulu katika masomo ya Sayansi Jamii umeoneshwa katika Jedwali Na. **6**.

**Jedwali Na. 6: Asilimia ya Ufaulu katika Masomo ya Sayansi Jamii**

| SOMO | MWAKA | IDADI | % waliopata A [75-100] | % waliopata A hadi B [65-100] | % waliopata A hadi C [45-100] | % waliopata A hadi D [30-100] | % waliopata F [0-29] |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Civics | 2022 | 633,095 | 0.50 | 1.77 | 11.25 | 31.12 | 68.88 |
| | 2023 | 694,373 | 0.72 | 2.96 | 18.19 | 48.27 | 51.73 |
| History | 2022 | 633,109 | 3.51 | 7.05 | 20.99 | 53.80 | 46.20 |
| | 2023 | 694,068 | 2.84 | 6.11 | 19.24 | 50.71 | 49.29 |
| Geography | 2022 | 633,140 | 4.00 | 9.10 | 27.80 | 55.00 | 45.00 |
| | 2023 | 694,237 | 2.43 | 6.40 | 24.66 | 53.78 | 46.22 |

(b) **Masomo ya Lugha**

Ufaulu wa somo la **Kiswahili** na **Chinese Language** ni mzuri sana ambapo katika somo la Kiswahili ni asilimia **95.18** na somo la **Chinese Language** ni asilimia **93.39**. Masomo ya **English Language** na **French Language** yana ufaulu wa wastani ambapo somo la **English Language** ni asilimia **68.27** na katika somo la **French Language** ni asilimia **55.61**. Aidha, somo la **Arabic Language** ufaulu unaendelea kuimarika kutoka asilimia **47.83** kwa mwaka 2022 hadi **48.72** kwa mwaka 2023.

Masomo ya **Chinese Language**, **Arabic Language** na **French Language** siyo masomo ya lazima kwa mwanafunzi ambapo yana idadi ndogo ya wanafunzi ambayo ni kati ya wanafunzi **1,921** hadi **10,269** sawa na asilimia kati ya **0.28** hadi **1.48** ya wanafunzi waliofanya Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili 2023. Mchanganuo wa masomo ya Lugha umeoneshwa katika Jedwali Na. **7**.

**Jedwali Na. 7: Asilimia ya Ufaulu katika Masomo ya Lugha**

| SOMO | MWAKA | IDADI | % waliopata A [75-100] | % waliopata A hadi B [65-100] | % waliopata A hadi C [45-100] | % waliopata A hadi D [30-100] | % waliopata F [0-29] |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kiswahili | 2022 | 633,253 | 12.47 | 29.51 | 75.28 | 95.66 | 4.34 |
| | 2023 | 694,400 | 4.24 | 14.19 | 64.15 | 95.19 | 4.81 |
| English Language | 2022 | 633,202 | 2.99 | 6.20 | 22.12 | 60.31 | 39.69 |
| | 2023 | 694,321 | 5.10 | 10.52 | 31.48 | 68.27 | 31.73 |
| French Language | 2022 | 9,222 | 1.94 | 4.25 | 16.51 | 50.95 | 49.05 |
| | 2023 | 10,269 | 5.91 | 10.97 | 29.28 | 55.61 | 44.39 |
| Arabic Language | 2022 | 2,116 | 2.79 | 6.57 | 24.15 | 47.83 | 52.17 |
| | 2023 | 2,506 | 3.71 | 8.46 | 27.85 | 48.72 | 51.28 |
| Chinese Language | 2022 | 1,561 | 8.20 | 16.40 | 49.58 | 89.81 | 10.19 |
| | 2023 | 1,921 | 18.32 | 34.31 | 67.52 | 93.39 | 6.61 |

(c) **Masomo ya Sayansi Asili, Hisabati na Teknolojia**

Ufaulu wa masomo ya **Biology**, **Engineering Science**, **Information & Computer Studies**, **Additional Mathematics** na **Home Economics** ni wa wastani ambao ni kati ya asilimia **55.74** hadi asilimia **70.29**.

Masomo ya **Physics**, **Chemistry**, **Agriculture** na **Basic Mathematics** yana ufaulu ulio chini ya wastani ambao ni kati ya asilimia **19.06** hadi **39.24**. Hata hivyo, ufaulu wa masomo ya **Physics**, **Agriculture** na **Basic Mathematics** umepanda kati ya asilimia **0.85** hadi **4.52**. Aidha, ufaulu wa somo la **Chemistry** umeshuka kwa asilimia **5.29** ikilinganishwa na ufaulu wa mwaka 2022.

Masomo ya **Agriculture**, **Engineering Science**, **Information & Computer Studies**, **Additional Mathematics** na **Home Economics** siyo masomo ya lazima kwa mwanafunzi ambapo yana idadi ndogo ya wanafunzi ambayo ni kati ya wanafunzi **441** hadi **27,022** sawa na asilimia kati ya **0.06** hadi **3.91** ya wanafunzi waliofanya Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili 2023. Mchanganuo wa masomo ya Sayansi Asili, Hisabati na Teknolojia umeoneshwa katika Jedwali Na. **8**.

**Jedwali Na. 8: Asilimia ya Ufaulu katika Masomo ya Sayansi Asilia, Hisabati na Teknolojia**

| SOMO | MWAKA | IDADI | % waliopata A [75-100] | % waliopata A hadi B [65-100] | % waliopata A hadi C [45-100] | % waliopata A hadi D [30-100] | % waliopata F [0-29] |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Physics | 2022 | 630,564 | 0.40 | 1.17 | 5.91 | 18.21 | 81.79 |
| | 2023 | 691,055 | 0.73 | 1.80 | 7.26 | 19.06 | 80.94 |
| Chemistry | 2022 | 632,840 | 1.79 | 3.94 | 13.71 | 33.45 | 66.55 |
| | 2023 | 694,343 | 1.98 | 4.00 | 12.30 | 28.16 | 71.84 |
| Biology | 2022 | 633,191 | 3.42 | 7.12 | 21.17 | 46.96 | 53.04 |
| | 2023 | 694,013 | 6.05 | 11.07 | 27.91 | 55.74 | 44.26 |
| Agriculture | 2022 | 23,870 | 0.94 | 2.94 | 15.30 | 38.88 | 61.12 |

| SOMO | MWAKA | IDADI | % waliopata A [75-100] | % waliopata A hadi B [65-100] | % waliopata A hadi C [45-100] | % waliopata A hadi D [30-100] | % waliopata F [0-29] |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2023 | 27,022 | 1.22 | 3.40 | 16.26 | 39.24 | 60.76 |
| Engineering Science | 2022 | 1,818 | 0.50 | 2.48 | 21.01 | 47.03 | 52.97 |
| | 2023 | 1,889 | 1.54 | 7.36 | 34.83 | 59.40 | 40.60 |
| Information & Computer Studies | 2022 | 12,862 | 3.42 | 10.90 | 35.04 | 59.73 | 40.27 |
| | 2023 | 14,731 | 4.47 | 13.03 | 41.93 | 67.62 | 32.38 |
| Basic Mathematics | 2022 | 633,185 | 1.96 | 3.30 | 8.15 | 16.56 | 83.44 |
| | 2023 | 694,275 | 4.67 | 7.08 | 13.42 | 21.08 | 78.92 |
| Additional Mathematics | 2022 | 398 | 6.53 | 16.58 | 52.26 | 76.88 | 23.12 |
| | 2023 | 441 | 16.78 | 28.12 | 51.70 | 70.29 | 29.71 |
| Home Economics | 2022 | 5,608 | 0.34 | 2.94 | 26.84 | 57.26 | 42.74 |
| | 2023 | 5,302 | 1.47 | 6.37 | 30.33 | 59.79 | 40.21 |

(d) **Masomo ya Biashara**

Ufaulu wa masomo ya **Commerce** na **Book-Keeping** ni wa wastani ambapo ufaulu wa somo la **Commerce** ni asilimia **50.28** na ufaulu wa somo la **Book-Keeping** ni asilimia **52.84**. Aidha, ufaulu wa somo la **Commerce** umepanda kwa asilimia **0.01** na ufaulu wa somo la **Book-Keeping** umepanda kwa asilimia **1.36**. Mchanganuo wa masomo ya Biashara umeoneshwa katika Jedwali Na. **9**.

**Jedwali Na. 9: Asilimia ya Ufaulu katika Masomo ya Biashara**

| SOMO | MWAKA | IDADI | % waliopata A [75-100] | % waliopata A hadi B [65-100] | % waliopata A hadi C [45-100] | % waliopata A hadi D [30-100] | % waliopata F [0-29] |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Commerce | 2022 | 74,040 | 3.54 | 8.53 | 26.31 | 50.27 | 49.73 |
| | 2023 | 70,704 | 3.86 | 9.83 | 29.03 | 50.28 | 49.72 |
| Book-Keeping | 2022 | 74,426 | 2.01 | 5.83 | 25.59 | 51.48 | 48.52 |
| | 2023 | 70,994 | 3.71 | 8.86 | 29.33 | 52.84 | 47.16 |

(e) **Masomo ya Utamaduni, Sanaa na Michezo**

Ufaulu wa somo la **Fine Art** na **Music** ni mzuri ambapo katika somo la **Fine Art** ni asilimia **81.89** na somo la **Music** ni asilimia **74.36**. Masomo ya **Physical Education** na **Theatre Art** yana ufaulu wa chini ya wastani ambapo somo la **Physical Education** ni asilimia **27.93** na katika somo la **Theatre Art** ni asilimia **48.95**. Hata hivyo, ufaulu wa somo la **Physical Education** umepanda kwa asilimia **20.35** na ufaulu wa somo la **Theatre Art** umepanda kwa asilimia **22.13** ikilinganishwa na ufaulu wa mwaka 2022.

Masomo ya **Utamaduni**, **Sanaa na Michezo** siyo masomo ya lazima kwa mwanafunzi ambapo yana idadi ndogo ya wanafunzi ambayo ni kati ya wanafunzi **273** hadi **7,282** sawa na asilimia kati ya **0.04** hadi **1.05** ya wanafunzi waliofanya Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili 2023. Mchanganuo wa masomo ya Utamaduni, Sanaa na Michezo umeoneshwa katika Jedwali Na. **10**.

**Jedwali Na. 10: Asilimia ya Ufaulu katika Masomo ya Utamaduni, Sanaa na Michezo**

| SOMO | MWAKA | IDADI | % waliopata A [75-100] | % waliopata A hadi B [65-100] | % waliopata A hadi C [45-100] | % waliopata A hadi D [30-100] | % waliopata F [0-29] |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Fine Art | 2022 | 1,242 | 0.48 | 3.62 | 43.24 | 87.92 | 12.08 |
| | 2023 | 1,496 | 1.07 | 6.89 | 49.87 | 81.89 | 18.11 |
| Music | 2022 | 411 | 7.54 | 10.71 | 25.06 | 34.31 | 65.69 |
| | 2023 | 273 | 26.37 | 32.97 | 56.78 | 74.36 | 25.64 |
| Physical Education | 2022 | 7,572 | 0.00 | 0.00 | 0.48 | 7.58 | 92.42 |
| | 2023 | 7,282 | 0.04 | 0.30 | 6.33 | 27.93 | 72.07 |
| Theatre Art | 2022 | 466 | 0.00 | 0.21 | 9.01 | 26.82 | 73.18 |
| | 2023 | 429 | 0.00 | 1.86 | 20.28 | 48.95 | 51.05 |

(f) **Masomo ya Ufundi**

Ufaulu wa masomo yote **manane** ; **Building Construction**, **Architectural Draughting**, **Civil Engineering Survey**, **Woodwork and Painting Engineering**, **Electrical Engineering**, **Electronics and Communications Engineering**, **Mechanical Engineering** na **Engineering Drawing** upo juu ya wastani ambapo ufaulu ni kati ya asilimia **57.98** hadi **77.85** na somo la **Electronics and Communications Engineering** lina ufaulu wa juu ambao ni asilimia **77.85** na somo la **Building Construction** lina ufaulu wa chini ambao ni asilimia **57.98** ikilinganishwa na ufaulu wa mwaka 2022.

Masomo ya **Ufundi** yana idadi ndogo ya wanafunzi ambayo ni kati ya wanafunzi **192** hadi **545** sawa na asilimia kati ya **0.03** hadi **0.08** ya wanafunzi waliofanya Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili 2023. Mchanganuo wa ufaulu wa masomo ya Ufundi umeoneshwa katika Jedwali Na. **11**.

**Jedwali Na. 11: Asilimia ya Ufaulu katika Masomo ya Ufundi**

| SOMO | MWAKA | IDADI | % waliopata A [75-100] | % waliopata A hadi B [65-100] | % waliopata A hadi C [45-100] | % waliopata A hadi D [30-100] | % waliopata F [0-29] |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Building Construction | 2022 | 510 | 0.59 | 2.16 | 23.73 | 55.49 | 44.51 |
| | 2023 | 545 | 0.00 | 3.30 | 30.28 | 57.98 | 42.02 |
| Architectural Draughting | 2022 | 490 | 0.41 | 1.22 | 15.10 | 40.61 | 59.39 |
| | 2023 | 526 | 1.52 | 7.22 | 33.84 | 58.56 | 41.44 |
| Civil Engineering Survey | 2022 | 336 | 0.00 | 1.49 | 17.86 | 48.51 | 51.49 |
| | 2023 | 281 | 1.07 | 3.20 | 35.94 | 61.57 | 38.43 |
| Woodwork and Painting Engineering | 2022 | 214 | 0.00 | 0.00 | 7.94 | 41.12 | 58.88 |
| | 2023 | 192 | 0.00 | 0.52 | 34.90 | 63.02 | 36.98 |
| Electrical Engineering | 2022 | 387 | 1.03 | 4.91 | 29.46 | 65.37 | 34.63 |
| | 2023 | 371 | 0.00 | 2.16 | 31.27 | 65.77 | 34.23 |
| Electronics and Communications Engineering | 2022 | 451 | 0.00 | 0.22 | 6.43 | 31.49 | 68.51 |
| | 2023 | 307 | 0.65 | 13.03 | 57.00 | 77.85 | 22.15 |

| SOMO | MWAKA | IDADI | % waliopata A [75-100] | % waliopata A hadi B [65-100] | % waliopata A hadi C [45-100] | % waliopata A hadi D [30-100] | % waliopata F [0-29] |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mechanical Engineering | 2022 | 424 | 0.24 | 1.65 | 32.31 | 70.05 | 29.95 |
| | 2023 | 381 | 1.84 | 15.22 | 56.69 | 75.07 | 24.93 |
| Engineering Drawing | 2022 | 479 | 5.64 | 15.24 | 49.06 | 72.86 | 27.14 |
| | 2023 | 431 | 2.78 | 14.39 | 47.33 | 73.55 | 26.45 |

(g) **Masomo ya Dini**

Ufaulu wa masomo ya **Bible Knowledge** na **Elimu ya Dini ya Kiislamu** ni mzuri ambapo ufaulu wa somo la **Bible Knowledge** ni asilimia **84.01** na ufaulu wa somo la **Elimu ya Dini ya Kiislamu** ni asilimia **68.32**.

Masomo ya **Dini** yana idadi ndogo ya wanafunzi ambapo katika somo la **Bible Knowledge** ni wanafunzi **22,175** (**3.21**%) na somo la **Elimu ya Dini ya Kiislamu** ni wanafunzi **87,272** (**12.63**%) ya waliofanya Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili 2023. Mchanganuo wa masomo ya Dini umeoneshwa katika Jedwali Na. **12**.

**Jedwali Na. 12: Asilimia ya Ufaulu katika Masomo ya Dini**

| SOMO | MWAKA | IDADI | % waliopata A [75-100] | % waliopata A hadi B [65-100] | % waliopata A hadi C [45-100] | % waliopata A hadi D [30-100] | % waliopata F [0-29] |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Bible Knowledge | 2022 | 20,527 | 1.78 | 9.40 | 47.34 | 73.60 | 26.40 |
| | 2023 | 22,175 | 13.12 | 34.48 | 70.20 | 84.01 | 15.99 |
| Elimu ya Dini ya Kiislamu | 2022 | 84,470 | 0.06 | 0.56 | 11.98 | 48.77 | 51.23 |
| | 2023 | 87,272 | 0.23 | 2.05 | 26.78 | 68.32 | 31.68 |

## 4.0 MATOKEO YALIYOFUTWA

Baraza la Mitihani limefuta matokeo yote ya wanafunzi;

(a) **178** waliofanya udanganyifu na **watatu** (**03**) waliandika matusi kwenye skripti zao katika Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne.

(b) **28** waliofanya udanganyifu na **14** waliandika matusi kwenye skripti zao katika Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili.

Matokeo hayo yamefutwa kwa mujibu wa Kifungu cha **5 (2) (j)** cha sheria ya Baraza la Mitihani sura ya **107** kikisomwa pamoja na Kifungu cha **30(2) (b) 2016** cha Kanuni za Mitihani.

## 5.0 PONGEZI ZA BARAZA

Baraza la Mitihani la Tanzania linapenda kuchukua fursa hii kuzipongeza Kamati za Uendeshaji Mitihani za Mikoa na Halmashauri/Manispaa/Jiji, Wakuu wa Shule, Wasimamizi na Wasahihishaji wa Upimaji uliyofanyika Oktoba/Novemba, 2023 kwa kazi kubwa na nzuri waliyoifanya katika kutekeleza jukumu la Uendeshaji Upimaji huo. Aidha, Baraza linawapongeza wanafunzi wote waliofanya Upimaji kwa kuwa na utulivu na kuzingatia taratibu za mitihani katika kipindi chote cha Uendeshaji wa Mitihani.

## 6.0 UPATIKANAJI WA MATOKEO

Matokeo ya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne na Kidato cha Pili (FTNA) iliyofanyika Oktoba/Novemba, 2023 yanapatikana katika tovuti zifuatazo:

- www.necta.go.tz,
- www.moe.go.tz,
- www.tamisemi.go.tz.

Dkt. Said A. Mohamed
**KATIBU MTENDAJI**
**07/01/2024**